# Asemavyo Mhariri:

## Maafisa Wa Vilabu Waonyesha Msimamo Wao

MAAFISA wa vilabu vya Mombasa wiki mbili zilizopita, walijiamulia kwa hiari yao wenyewe kuwarudisha akina **Sadia Khamis** na kundi lake katika kuongoza kandanda wilayani Mombasa wakati wa Mkutano Mkuu wa Shrikisho la Soka (KFF) tawi dogo la Mombasa uliofanyika kwenye ukumbi wa Tusker. Vilabu vipatavyo 62 kati ya vilabu 67 vilishiriki uchaguzini.

BILA shaka ushindi huo wa Sadia Khamis pamoja na viongozi wengine waliochaguliwa katika kundi lake, umedhihirisha wazi kwamba vilabu bado vingali na imani ya maongozi yao na ndipo wakatumia haki yao ya kuwachaguwa viongozi bila ya kushawishiwa wala kushurutishwa.

KUTOKANA na utafiti nilioufanya kabla na wakati wa uchaguzi huo, nimegundua kuwa maafisa wa vilabu walikuwa wameshaamua ni akina nani wanawataka kuendesha soka hapa wilaynai Mombasa na ndipo wakati ulipowadia, wakajipanga mlolongo mkubwa kwa upande wa wale walioshinda.

UAMUZI nilofikia ni kwamba uchaguzi huo uliendeshwa kihalali na Naibu Katibu wa Shirikisho la Soka (KFF) makao makuu, **Bw. Victor Mbaji** ambaye alifuata kanuni na katiba ya KFF. Ingawa kulikuwa na mvutano wa makundi mawili, Bw. Mbaji alisimamia haki na kuweza kuendesha uchaguzi na viongozi waliochaguliwa wakakabidhiwa tena madaraka yao.

KAMA kuna madai ya kuwa labda kulikuwa na viongozi "bandia" kwenye ukumbi huo, je, ni kwa nini waliotoa madai hayo hawakuondoka na kudai uchaguzi haukuwa wa halali? Kwa nini walikubali kupendekezwa kama wapigania viti, waliowaunga mkono wakapiga foleni nyuma yao? Kwa nini hawakupinga hadi dakika ya mwisho wakafahamisha uchaguzi haukuendeshwa kihalali?

Hii ilidhihirisha wazi kuwa kusimama kwao, kupendekezwa kwao na wafuasi wao na kusimama mbele wakifuatiwa na wafuasi wao, walikuwa wamekubali wajumbe waliokuwako mkutanoni walikuwa ni maafisa halali wa vilabu na wamekubali kusimama na kuvipa ruhusa vilabu kuteua viongozi wanaowataka. Hawana budi kukubali kushindwa kama wanamichezo na wangoje wakati mwingine wajaribu bahati yao.

SEHEMU zote za Pwani zimekamilisha uchaguzi wa matawi madogo ya wilaya na uchaguzi unaosubiriwa kwa hamu zaidi ni ule wa KFF Pwani. Lazima viongozi waliokuwako wapime kila mtu na kazi ambayo ameitimiza wakati wake. Hatutaki makosa ya kuchaguwa mtu kwa ajili ya jina pekee bali tunahitaji mtu wa kazi anayoifanya.

KAMA mtu alikuwa hakutimiza wajibu wake ipasavyo bali amekalia kiti kwa sababu ya jina pekee, basi mtu huyo awekwe kando na yule ambaye alihudumia madaraka hayo kwa kazi bali si cheo, basi yule aliyefanya kazi za mwingine astahili kupowa madaraka- **ABDULRAHMAN SHERIFF**

MAISHA - MTUKUFU Rais Moi akiwa pamoja na Miamba ya Harambee Stars baada ya kulibeba kombe la Challenge kwa mwaka watatu mfululizo. Kombe hilo litabaki Kenya milele.

PICHA: KENYA NEWS AGENCY

# LEA MWANA MWEMA NA MUI NAE PIA

SINA budi kutoa shukrani nyingi sana kwa Mhariri wa Kiswahili katika gazeti hili tukufu la *COASTWEEK*, Bw. Abdulrahman Sheriff kwa makala yake ya "Asemavyo Mhariri" ambayo alizungumzia juu ya akina Kudura, Kido wasaidiwe...

Namtolea pongezi nyingi Bw. Sheriff kwa kugundua yale aliyoyasema juu ya maonevu yanayofanywa na Wizara ya Habari na Utangazaji kuhusiana na mambo kadha ya kundi la Akina Kudura, Kido na wengineo ndio wanaowafurahisha zaidi wale watazamaji wa vipindi vya kwenye televisheni lakini ni ajabu kwa nini hawahudumiwi ipasavyo.

## KUDURA

Bila shaka wasomaji wenzangu watakubaliana nami kuwa kina Kido, Kurura, Mashaka na wengineo wanapotayarisha vipindi vyao huwa vya kuvutia kuliko vile vinavyotayarishwa huko Nairobi lakini ajabu wale wa Nairobi ndio wanaokula vitamu.

Shirika la Kenya Film Corporation lazima lifanye mipango ya kuwakusanya Wanakenya wanaofanya michezo ya kuigiza pamoja ili watayarishe sinema ambazo zitawafaidi wananchi badala ya kutuletea sinema ambazo zinawaharibu watoto wetu.

Umefika wakati KFC wapigishe sinema zenye manufaa kama zile zinazowashirikisha akina Kido ili watoto wetu wanaoinukia

## UHUNI

wapate kujitunza mema badala ya kuiga maovu ambayo mwisho ndipo wanainukia na uhuni wa kupindukia.

*JOHNSON MWERO KULAMBA,*
*S.L.P. 86333,*
*MOMBASA.*

MAOMBI-MTUKUFU Rais Daniel arap Moi akihudhuria kwenye ibada katika kanisa la African Inland Church

PICHA: KENYA NEWS AGENCY

SHUKRANI-WAZIRI wa Ardhi na Makao, Bw. Paul Ngei (kushoto) anamshukuru Balozi wa Uingereza nchini Kenya, kwa zawadi yake ya Mzinga wa Asali wakati alipomtembelea afisi yake mjini Nairobi.

PICHA: KENYA NEWS AGENCY

# Heko Madiwani Voi

*Napenda kuunga mkono madiwani wa Voi kwa juhudi zao za kuanzisha uwanja wa michezo ambao hivi sasa unatengenezwa.*

*Kutokana na maendeloo haya mji wa Voi hivi sasa unaendelea kupanuka. Wakati huo huo ningependa kuwapongeza polisi wa Voi kwa kazi yao nzuri wanayotekeleza kwa kuwalinda wananchi wa Voi ambapo mpaka hivi sasa hatujapata kusikia habari mbaya za uhalifu au ajali mbaya.*

*Hata hivyo ningependa kuwaomba madereva wa matatu waache mtindo wa kuwalaghai abiria kutoka Taita juu kwamba wanakwenda Mombasa na hali wakifika Voi wanabadilisha nia na kushia hapo.*

*Hali hii imeleta shida sana kwa wanawake na watoto na hata vitu vyao kupotea safarini.*

**Mnyika M. Mwaigho**
**Magongo, Mombasa.**

# Farucci Coastweek

JISHINDIE VIATU MARIDADI
VYA FARUCCI KWA MSHINDI
WA KWANZA NA T-SHIRT
KWA WASHINDI WA PILI
NA WATATU KATIKA SHINDANO
JIPYA LA KUJAZA MANENO

## SWAHILI CROSSWORD No. 177

*KWENDA KULIA:*

1. Anayetengeneza vyombo kwa kutumia udongo.
5. Kipimo cha eneo la yadi 4840 za mraba. (Imezidi A)
7. Nyumba hizi ni ... nani?
8. United Nations.
9. ....... ndiye mwenye.
12. Kama, mfano.
13. Waweke Sawa.
15. Mateka.
16. Mwanya, mpasuko.

*KWENDA CHINI:*

1. Bomba la maji.
2. Wingi wa wangwa.
3. Sadiki, kubali.
4. Babaisha, Sumbua.
6. Tazama, kagua, pima shamba.
10. Fimbo upande mmoja uliyovimba.
11. Sema, fahamisha.
13. Washa, doa.
14. Sehemu ya usoni.

**Wshindi wa Fumbo La Kujaza maneno No. 176.**

1. Sharifa A. Mohamad, Sanduku La Posta 80306, MOMBASA.

2. Ndan A. Abwonyo, Sanduku La Posta c/o KH. S. S. Kibiringo Box 85521, MOMBASA.

3. RIZIKI DOLLAR, Sanduku La Posta 84572, MOMBASA.

*Washindi waombwa wafike afisini mwa COASTWEEEK.*

**MAJIBU YA SHINDANO LA FUMBO LA KUJAZA MANANO No. 176.**

*KWENDA KULIA*

1. RUNINGA, 6. SUI, 7. MAONI, 8. MALI, 10. AMANI, 13. IDI, 15. SEBULE, 16. TUNU, 17. WAPIKE.

*KWENDA CHINI*

1. RAMBA, 2. NGOMA, 3. NDIMI, 4. ASALI, 5. KIA, 9. IDHINI, 11. MBEGA, 12 NYUNI, 14. PETE.




**JINA**.........................................

**SANDUKU LA POSTA**..............................

.................................................

**Shindano la Fumbo La kujaza Maneno:—**

Uamuzi wa majaji utakuwa wa mwisho. Hakuna malalamiko yoyote yatakayokubaliwa. Washindi watatu kila baada yawiki mbili watapata viatu na T-Shirt maridadi. Shindano hili limedhaminiwa na COASTWEEK limited Mombasa.

Jawabu za fumbo hili lipelekwe kwa Muhariri COASTWEEK, Sanduku la Posta 87270, Mombasa, Kenya Siku ya jumatano tarehe **Jan. 11, 1984.** Saa nne asubihi shindano hili litakuwa mwisho.